

INS-A003- UNYANYASAJI WA MWANAFUNZI VITISHO, UONEVU, UNYANYASAJI WA MTANDAONI, NA VURUGU KWENYE URAFIKI WA MAPENZI KWA VIJANA

SERA YA UTAWALA

MAELEKEZO

MUHTASARI

Wilaya ya shule za Salem-Keizer imejidhatiti kutoa mazingira ambayo wanafunzi wanaweza kusoma, kushiriki katika shughuli zinazofadhiliwa na wilaya na kufanya kazi katika mazingira ambayo hayana unyanyasaji, vitisho, uonevu, unyanyasaji wa mtandaoni na vurugu kwenye urafiki wa mapenzi kwa vijana

MAANA

Wilaya ya shule

Inajumuisha majengo ya wilaya, maeneo ya wilaya na mali isiyo ya wilaya na kama mwanafunzi yupo kwenye shughuli au kazi yoyote inayofadhiliwa na wilaya, iliyoidhinishwa na wilaya, au shughuli yeyote, kama vile safari za shule au shughuli za michezo ambapo wanafunzi wapo chini ya mamlaka ya wilaya ya shule.

Mtu wa Mwingine

Inajumuisha, lakini siyo tu, makocha, wanaojitolea kwenye shule, wazazi, wageni, wakandarasi wa huduma, au wengine wanaohusika katika biashara na wilaya, kama mfanyakazi wa biashara au mashirika yanayoshiriki katika programu na Wilaya na wengine ambao sio chini ya udhibiti wa wilaya moja kwa moja kwenye muingiliano wa mashindano ya kimichezo na wilaya nyingine.

Uonevu

Inajumuisha, lakini sio tu, kitendo chochote ambacho kinahatarisha afya ya akili, afya ya mwili au usalama wa mwanafunzi kwa madhumuni ya kuanzishwa au kama sharti la kupata uanachama katika au ushirika na, shughuli yoyote inayofadhiliwa na wilaya au kiwango cha darasa (yaani, utumwa wa kibinafsi, kulisimua kijinsia/unyanyasaji wa kijinsia, unywaji wa kulazimishwa na kinywaji chochote, kinywaji cha pombe, dawa za kulevya au dutu inayodhibitiwa, kulazimishwa kutengwa kwa muda mrefu kutoka kwenye mawasiliano ya kijamii, kunyimwa usingizi au shughuli nyingine yoyote ya kulazimishwa ambayo inaweza kuathiri vibaya afya ya akili au mwili au usalama wa mwanafunzi); inahitaji, inahimiza inaidhinisha au inaruhusu mwingine kuwa chini ya kuvaa au kubeba nakala yoyote chafu au mzigo wa mwili; au ugawaji wa mizaha itakayofanywa au shughuli zingine kama hizo zinazokusaidia kudhalilishwa au kudhalilisha. Sio utetezi dhidi ya uonevu kwamba mwanafunzi aliyefanyiwa kukubali uonevu au kukubali uonevu.

Unyanyasaji, Vitisho, Uonevu

Kitendo chochote ambacho kinaingilia kwa kiasi kikubwa manufaa ya elimu ya mwanafunzi, fursa au utendaji, ambao hufanyika kwenye, au mara moja karibu na au karibu kabisa na uwanja wa shule ya wilaya, kwenye shughuli yoyote ya wilaya, kwenye usafiri unaotelewa na wilaya, kwa kundi linalolindwa na sheria na ina athari ya:

- Kumuumiza mwanafunzi au kuharibu mali za mwanafunzi.
- Kwa kujua na kumweka mwanafunzi kwenye hofu ya kuumizwa au kwa kuharibu mali za mwanafunzi; au
- Kutengeneza mazingira ya vitisho kwenye elimu, inajumuisha kuingilia kwenye kisaikolojia ya ustawi kwa mwanafunzi

Unyanyasi wa mtandaoni

Kutumia vifaa chochote cha kieletronika kunyanyasa, kutishia au kuonea. Mawasiliano ya namna hii ambayo yanatokea nje ya viwanja shule lakini vinaweza kuingilia au kuzuia mazingira mazuri ya kujifunza yanaweza pia kuzingatia.

Kutisha

Kitendo chochote kinachopelekea mfanyakazi wa wilaya, mwanafunzi au mtu mwingine kwenye kutishiwa hofu na kuumizwa vibaya.

Mahusiano au Urafiki wa Mahusiano

Mahusiano yeyote ya urafiki au urafiki wa mapenzi kati ya watu wawili. Hii haijumuishi urafiki wa kawaida au udugu kati ya watu wawili kwenye biashara au mitandao ya jamii.

Vurugu za Mahusiano ya Kimapenzi kwa Vijana

Mwenendo wa tabia ambayo mtu hutumia au kutishia kutumia unyanyasaji wa mwili, kiakili au kihemko kumdihibiti mtu mwingine; au tabia ambayo mtu hutumia au kutishia kutumia unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya mtu mwingine ambaye yuko kwenye uhusiano wa kimapenzi ambapo mtu mmoja au wote wawili wana umri wa miaka 13 hadi 19.

Ukatili wa Nyumbani

Unyanyasaji katika familia na wanafamilia inayofafanuliwa katika Sheria Iliyorekebisha ya Oregon 107.705.

Kundi Linalolindwa

Ina maana iliyofafanuliwa katika Sheria Iliyorekebisha ya Oregon (ORS) 339.351(3): Kundi la watu wanaotofautishwa, au wanaoonekana kutofautishwa, kwa rangi, dini, jinsia, mwelekeo wa kijinsia, utambulisho wa kijinsia, asili ya kitaifa, hali ya ndoa, hali ya familia, chanzo cha mapato au ulemavu

Mwelekeo wa Kijinsia

Jinsia halisi au inayoonekana ya mtu tofauti, ushoga, jinsia mbili.

Utambulisho wa Jinsia

Utambulisho wa mtu binafsi unaohusiana na jinsia, muonekano, usemi au tabia bila kujali kama utambulisho, muonekano, usemi au tabia inatofautiana na ile inayohusishwa na jinsia aliyopewa na mtu huyo wakati wa kuzaliwa.

Kulipiza Kisasi

Vitendo vyovyote ikiwa ni pamoja na lakini sio tu uonevu, unyanyasaji, vitisho au uonevu, au unyanyasaji wa mtandaoni kwa mwathiriwa, mtu kwa kujibu ripoti halisi au dhahiri, au kushiriki katika uchunguzi wa uonevu, unyanyasaji, vitisho au uonevu, vitisho, vitendo vya unyanyasaji wa mtandaoni, au kulipiza kisasi.

MAELEKEZO

1. Wanafunzi wanategemewa kuwa na heshima ambayo inakuza mazingira mazuri ya elimu
2. Uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao na wanafunzi, wafanyakazi au mtu mwingine kuelekezea wanafunzi ni marufuku.
3. Msimamizi wa shule atapokea ripoti na kuchunguza mara moja vitendo vyovyote vilivyoriipotiwa vya uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji kwenye mtandao kulingana na taratibu zilizotengenezwa na Msimamizi wa mashule
 - a. Mfanyakazi yeyote yule mwenye kujua ukiukwaji wa sheria anatakiwa kutoa taarifa ya wasiwasi kwa msimamizi wa shule ambaye ana jukumu kwa jumla la uchunguzi wote.
 - b. Kushindwa tutoa taarifa ya vitendo vya uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao kwa msimamizi wa shule kunaweza kufanya kuchukuliwa hatua za kurekebisha, na hata kuachishwa kazi. Hatua za marekebisha hazitakuwa tu kwenye ripoti isiyojulikana.
 - c. Mwanafunzi yeyote yule anayejua mwenendo wa ukiukwaji wa hii sera au kuhisi amefanyiwa kitendo cha uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao kwa kukiuka sera hii, anahimizwa kuripoti mara moja wasiwasi wake kwa msimamizi wa shule ambaye ana jukumu la uchunguzi wote.
 - d. Mtu mwingine yeyote yule mwenye kujua mwenendo wa ukiukwaji wa sheria hii anahimizwa kutoa ripoti wa wasiwasi kwa msimamizi wa shule.

- e. Taarifa itakayotolewa na mwanafunzi au mtu wa kujitolea inaweza kuwa isiyokuwa na jina la kumtambua mtu. Mwanafunzi au mtu wa kujitolea anaweza pia kutoa wasiwasi wake kwa mwalimu au mshauri wa wanafunzi ambaye atakuwa na jukumu la kumjulisha msimamizi wa shule.
 - f. Ripoti kuhusu mwalimu mkuu inaweza kujazwa kwa Idara ya Mwajiri au Mkuu wa mashule.
 - g. Ripoti kuhusu Mkuu wa mashule inaweza kujazwa kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Shule.
 - h. Mfanyakazi yeyote, mwanafunzi au mtu mwingine kumshatikia mtu uongo uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao atakabiliwa na matokeo na hatua zinafaa za kurekibisha
 - i. Kama ripoti inahusisha Ishara ya chuki au nembo ya chuki, msimamizi wa shule atafuata hatua kama zilivyoainishwa kwenye sera ya ADM-A012 – Matukio ya Upendeleo na Nembo ya Chuki
 - j. Ikiwa ripoti inahusisha vitendo ambavyo vitakiuka Title IX, msimamizi wa shule atawasiliana na Mratibu wa Wilaya ya Shule wa Title IX
4. Msimamizi wa shule atawa taarifu wazazi au walezi wa mwanafunzi ambaye alikuwa chini ya kitendo cha uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao, na wazazi au walezi wa mwanafunzi ambaye amefanya kitendo cha uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana au na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao kulingana na utaratibu kwenye INS-P006 Uchunguzi wa Ripoti ya Mwanafunzi Unyanyasaji, Vitisho, Uonevu, Unyanyasaji wa Mtandao na Vurugu za Mahusiano ya Vijana.
 5. Wanafunzi ambao tabia zao zitapatikana kuwa zinakiuka sera hii watakabiliwa na matokeo na hatua zinazofaa za kurebisha ambazo zinaweza kujumuisha hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sera na utaratibu wa nidhamu ya wanafunzi kwenye wilaya ya shule.
 6. Wafanyakazi ambao tabia zao zimepatikana kuwa zinakiuka sera hii watakabiliwa na matokeo na hatua zinazofaa za kurekebisha ambazo zinaweza kujumuisha hatua ya kinidhamu, hadi kujumuisha kufukuzwa.
 7. Watu wengine ambao tabia zao zimepatikana kuwa zinakiuka sera hii wanaweza kukabiliwa na hatua za vikwazo kama zinavyoelezewa na Mkuu wa mashule
 8. Wanafunzi, wafanyakazi, au mtu mwingine anaweza pia kupelekwa kwa maafisa wa sheria na usalama.
 9. Uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao kulipiza kisasi dhidi ya mtu yeyote ambaye ni mwathirika wa, mtu aliyetoa ripoti, ambaye anadhaniwa kuripoti, au kuwasilisha malalamiko uonevu, unyanyasaji, vitisho, vurugu za mahusiano ya vijana na vitendo vya unyanyasaji wa kwenye mtandao au vinginevyo kushiriki katika uchunguzi au uchunguzi ni marufuku kabisa. Mtu anayejihusisha na tabia ya kulipiza kisasi atakubaliwa na matokeo sahihi
 10. Mtu anaweza kuomba Wilaya ya shule kupitia hatua zilizochukuliwa na mfanyakazi katika kujibu na/au kuchunguza ripoti kwa kuwasilisha ombi la maandishi kwa Mkuu wa mashule. Maombi yatumwe ndani ya siku 10 za kazi baada ya mtu kupokea taarifa ya matokeo ya uchunguzi.
 11. Taarifa kuhusiana kwa kuzuia, na majibu sahihi, vitisho, vitendo vya uonevu, unyanyasaji kwenye mtandao, vurugu za mahusiano ya vijana na unyanyasaji majumbani zitajumuishwa katika programu za mafunzo kwa wanafunzi na wafanyakazi wa wilaya ya shule.
 12. Msimamizi wa mashule atakuwa na jukumu la kuhakikisha kuwa kwa kila mwaka tangazo la sera hii inatolewa kwenye kijitabu cha mtaala wa mwanafunzi na mfanyakazi, kwenye tovuti ya wilaya ya shule, na shule na ofisi za wilaya ya shule. Nakala ya sera hii walau iwe na ukubwa 8.5" x 11" ipandikwe kwenye shule za sekondari pamoja na high skuli.
 13. Kama inavyotakiwa na ORS 339.368, mabango yaliyotolewa na Idara ya Elimu ya Oregon kuhusu unyanyasaji wa nyumbani itabandikwa katika maeneo yanayooneka wazi katika jengo la shule.
 14. Wilaya ya shule imepitisha sera tofauti ya Unyanyasaji wa Kijinsia.
 15. Msimamizi wa shule na Mkuu wa mashule wana jukumu la kuhakikisha kuwa sera hii inatekelezwa.

MATUMIZI

- Hii sera inatumika kwa wanafunzi, wafanyakazi, wajumbe wa bodi ya shule, na wengine wanaohusika.

NYARAKA ZINAZOHUSIANA

- INS-P006 – Uchunguzi wa Ripoti ya Uonevu, Unyanyasaji, Vitisho, Unyanyasaji kwenye mtandao na Vurugu za Mahusiano ya Vijana
- ADM-A012 – Matukio ya Upendeleo na Alama za Chuki
- HUM-A029 – Unyanyasaji wa Kijinsia

MAMLAKA YA IDHINI

- Mwaajiri

HISTORIA YA MAREKEBISHO

- 07/11/2022 – Sera imeundwa na kuidhinishwa
- 12/06/2024 – Imesasishwa kwa templeti inayoweza kufikiwa na kufuata mahitaji ya ORS 339.356
- 03/26/2026 – Ufafanuzi ulioongezwa na taarifa kwa Mratibu wa Title IX